1.0: Utangulizi

Wilaya ya Kwimba ni moja wapo ya Wilaya kongwe kati ya Wilaya saba za Mkoa wa Mwanza. Katika kuhakikisha kuwa huduma muhimu zikiwemo za utawala zinasogezwa karibu na wananchi, mwaka 1973 Serikali iliigawa Wilaya ya Kwimba na kuanzisha Wilaya mbili za Kwimba na Magu. Pia mwaka 1996 Wilaya ya Kwimba iligawanywa na kuwa Wilaya ya Misungwi na Kwimba ya sasa.

1.1: Mahali ilipo

Wilaya ya Kwimba ipo kwenye latitudo 2° 45’ na 3° 53’ Kusini mwa Ikweta na longitudo 33° na 33° 30’ Mashariki mwa Meridiani. Kaskazini Wilaya imepakana na wilaya ya Magu, Mashariki inapakana na wilaya ya Maswa, Kusini inapakana wilaya ya Kishapu na Shinyanga Vijijini na upande wa Magharibi imepakana na wilaya ya Misungwi.

1.2: Eneo na Maeneo ya Utawala

Wilaya ya Kwimba ina eneo la kilometa za mraba 3,903, ina Tarafa tano (5), Kata 30, Vijiji 119, Vitongoji 871 na Mamlaka ya Mji Mdogo. Pia ina majimbo mawili (2) ya Uchaguzi wa Bunge na Madiwani ambayo ni Kwimba na Sumve. Makao Makuu ya Wilaya ni Ngudu yaliyo umbali wa kilomita 98 kutoka makao makuu ya Mkoa wa Mwanza.

1.3: Idadi ya Watu.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, wilaya Kwimba ilikuwa na jumla watu 406,509 kati ya hao wanawake 198,096 na wanaume 208,414. Ongezeko la watu kwa mwaka ni 1.9% na ujazo wa watu kwa kilomita za mraba 106. Kwa sasa wilaya inakadiliwa kuwa na watu 462,663 kati yao wanaume ni 237,203 na wanawake 225,460 (makisio ya takwimu ya Taasisi ya Taifa kuishia mwezi Desemba 2016)

1.4: Hali ya Hewa.

Wilaya ya Kwimba kwa sehemu kubwa ni tambarare, mabonde na miinuko michache na vilima vya hapa na pale. Hali ya hewa ya Wilaya hii ni ya ukame kwa ujumla, ambapo mvua ni haba, haziaminiki au kutabirika kwa urahisi. Wastani wa mvua kwa mwaka ni milimita 700-1200. Kiwango cha joto ni nyuzi 25^0-33^0C kwa mwaka; na pepo kavu karibu mwaka wote. Majira ya hali ya hewa yamegawanyika katika sehemu kuu tatu yaani majira ya mvua ya muda mfupi (vuli) ambayo huanza katikati ya Oktoba hadi Desemba, majira ya kipindi kirefu cha mvua (masika) ni katikati ya Februari hadi Mei na majira ya kipindi kirefu cha jua ni kati ya Juni hadi katikati ya Oktoba.

2.0: HISTORIA YA KILIMO CHA ZAO LA PAMBA WILAYANI KWIMBA

Pamba ni zao kuu la biashara katika wilaya ya Kwimba zaidi ya asilimia 70 ya wakulima walikuwa wanajishughulisha na kilimo cha pamba. Kwa kipindi cha miaka mitatu zao la pamba limekuwa likishuka uzalishaji kama ifuatavyo; mwaka 2014/2015 uzalishaji ulikuwa kilo 7,596,916, 2015/2016, kilo 4,512,420 na 2016/2017 kilo 2,051,122.

Katika vipindi vyote hivi vitatu kulikuwepo na mafanikio na changamoto mbalimbali zilizojitokeza. Mafanikio machache yaliyopatika kupitia kilimo cha pamba kwa mkataba ni upatikanaji wa pembejeo kwa mkopo, uwezeshwaji wa huduma za ugani kutoka kwa makampuni na uundaji wa Vikundi vya wakulima (FBGs). Mbali na mafanikio machache kulikuwa na changamoto zilizokwamisha kilimo cha mkataba zikiwemo; **ukopeshwaji usio fuata taratibu, urejeshwaji mdogo wa madeni, pembejeo zisizo na ubora, makampuni kushindwa kutimiza masharti ya mkataba, bei ya dogo ukilinganisha na gharama za uzalishaji na mvua zenye mtawanyiko usioridhisha.**

3.0: UTEKELEZAJI WA KILIMO CHA PAMBA KWA MKATABA MSIMU 2016/17

Katika msimu wa kilimo cha pamba 2016/17, Wilaya ya Kwimba imeitikia wito wa Mhe.Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufufua zao la pamba ambalo kwa takribani miaka mitano uzalishaji wake umeshuka. Lengo ni kuwezesha uzalishaji mkubwa wa pamba kama malighafi wenye tija ili kuwezesha uendeshaji wa viwanda.Kwa kutambua kuwa zao hili lina mnyororo mrefu wa thamani.

Katika kutekeleza agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John .V.K.Mongella, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza aliagiza Wakuu wa Wilaya kuhakikisha zao la pamba linafufuliwa kwa kuongeza tija na uzalishaji. Wilaya ya Kwimba iliandaa andiko lenye vigezo na masharti ya kuwekeza katika kilimo cha pamba na kulituma kwa Makampuni 13 ambayo ni Afrisian Ginning, SM Holdings, ICK Cotton, Kahama Oil Mills, Kahama Cotton Company, Alliance Ginneries, Birchad Oil Mills, Olam (T), Aham Investment Co. Ltd, Fresho Investment, Gaki Investment Co. Ltd na Nida Textile Mill. Makampuni hayo yalitumiwa mwaliko wa kuomba kuwekeza katika kilimo cha pamba kwa mkataba kuanzia msimu 2016/2017. Kati ya makampuni 13 ni makampuni matatu (3) ambayo ni SM Holdings, Afrisian Ginning na ICK Cotton ziliomba kuwekeza na baadaye Halmashauri ilifunga mkataba na kampuni hizo kwa kipindi cha miaka mitatu.

4.0: MIKAKATI ILIYOTUMIKA KUFANIKISHA KILIMO CHA MKATABA

1. Timu za uhamasishaji wa ngazi ya Wilaya kupita kila kijiji kuelemisha na kuamsha ari ya kufufua kilimo cha pamba walau kila kaya kulima ekari moja.
2. Ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika shughuli za kilimo cha pamba hususan Bodi ya Pamba, TGT na wataalam kutoka kampuni Quton.
3. Kugawa maeneo ya uwekezaji kwa kuzingatia mahitaji ya Kampuni; SM Holdings tarafa ya Ibindo, Afrisian Ginning tarafa ya Mwamashimba na ICK Cotton tarafa ya Nyamilama, Ngudu na Ngulla. Lengo la Wilaya kugawa uwekezaji kwa maeneo ni kuondoa muingiliano na utegeaji katika uwekezaji.
4. Uundwaji wa Vikosi Kazi ngazi ya Wilaya na Vijiji kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa kilimo cha pamba.
5. Kuboresha huduma za ugani kwa kuwapa maafisa ugani pikipiki, mafuta na posho kwa ajili ya kusimamia majukumu yao.
6. Kuanzisha shamba darasa la viongozi wa kamati ya Ulinzi na Usalama na Wakuu wa Idara wa Halmashauri ili kuhamasisha jamii kutekeleza kilimo cha Pamba.
7. Kuanzisha mashamba darasa katika shule za msingi na Sekondari ili kufufua elimu ya kujitegemea shuleni na kuandaa wakulima wa baadaye.
8. Usimamizi thabiti wa utekelezaji wa majukumu yaliyoanishwa kwenye mkataba.

5.0: HALI YA USAMBAZAJI PEMBEJEO

Kwa msimu 2016/17, Wilaya ilipata mgawo wa mbegu tani 500 UK 91(manyoya) kutoka Bodi ya pamba. Kutokana na mahitaji kuongezeka hadi kumalizika kwa msimu wa kupanda jumla ya tani 518 za UK 91 na tani 80 za UKM08 (kipara) zilisambazwa vijijini. Kati ya mbegu hizo jumla ya tani 488 za UK 91 na tani 78 za UKM08 zilichukuliwa na wakulima. Makisio ya ekari zilizotarajiwa kulimwa zilikuwa ni ekari 61,873.

Kutokana na changamoto ya hali ya hewa ilisababisha wakulima kulazimika kupanda zaidi ya mara moja na wengine kushindwa kabisa kupanda. Makisio yalishuka hadi kufikia ekari 46,000. Hata hivyo katika zoezi la uhakiki wa mashamba ambalo limekamilika mwezi Machi, jumla ya ekari 24,025 zimebainishwa kupandwa na kuota vizuri.

Kulingana na makisio ya ekari 61,873 ambazo zilitokana na usambazaji wa mbegu, mahitaji ya viuadudu yalikuwa chupa 165,000. Hadi kufikia sasa ni chupa 59,040 ambazo zimesambazwa vijijini, kati ya viuadudu hivyo chupa 46,840 zimetolewa na makampuni, chupa 11,500 zimetolewa na CDTF na chupa 700 zimetolewa na Bodi ya Pamba. Kwa upande wa vinyunyizi jumla ya vinyunyizi 189 vimesambazwa na vinyunyizi 148 vimechukuliwa na wakulima.

5.1: Ukopeshwaji wa pembejeo kwa kila kampuni

KAMPUNI	MBEGU				

	UK 91	UK M08	**DENI LA MBEGU (TShs)**	**VIUADUDU (CHUPA)**	**DENI LA VIUADUDU**	**WAKULIMA WALIOKOPA MBEGU** (Idadi)
SM HOLDINGS	91,387	47,856	173,760,500/=	14,068	28,136,000/=	5,472
I.C.K COTTON	227,237	0	167,070,128/=	22,803	45,606,000/=	5,493
AFRISIAN GINNING	123,650	30,178	104,415,500/=	10,034	20,068,000/=	3,193
JUMLA	**442,276**	**77,396**	**444,618,128/=**	**46,905**	**93,810,000/=**	**14,158**

Jumla ya Tsh 538,428,128.00 zimewekezwa na makampuni matatu zikiwa ni gharama ya mbegu na viuadudu.

6.0: UWEZESHWAJI WA SHUGHULI ZA KILIMO CHA PAMBA KWA MKATABA.

Katika kuendesha shughuli za kilimo cha pamba kwa mkataba, Halmashauri imechangia shilingi milioni 7.3 ambazo zilitumika katika zoezi la uhamasishaji wa kilimo cha pamba kwa kununua mafuta ya dizeli na petroli. Wilaya ilipokea pikipiki 10 na shilingi milioni 12 kutoka kwa makampuni, Shirika lisilokuwa la kiserikali la Gatsby Africa liliwezesha shilingi milioni 8. Fedha hizo zimekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha shughuli za kilimo cha pamba hususan katika mambo yafutayo;

1. Posho ya nauli na mafuta kwa maafisa ugani, uendeshaji wa vikao vya kazi vya maafisa ugani ambavyo vimeweza kufanyika mara mbili, hii ni katika kuhakikisha kuwa elimu ya kilimo bora cha pamba inawafikia wakulima kwa wakati
2. Kusimamia zoezi la uhakiki wa mashamba yaliyolimwa na kuota vizuri
3. Mafuta ya dizeli kwa ajili ya maafisa kilimo wilayani na wajumbe wa DTF kufika vijijini kufuatilia taarifa mabalimbali za maendeleo ya

kilimo na kufanya mazunguzo na Vikosi kazi vya pamba vya vijiji na wakulima.

7.0: **MAFANIKIO KUPITIA KILIMO CHA PAMBA KWA MKATABA.**

1. Ushirikiano mzuri baina ya viongozi ngazi zote Wilayani zimeleta matarajio makubwa ya kufufua zao la pamba.
2. Mwitikio mkubwa wa wakulima kulima pamba bila kukata tamaa kwa changamoto ya hali ya hewa.
3. Kumekuwepo na msingi mzuri wa VTF, katika kuunda na VTF kutambua wajibu wao katika kusimamia usambazaji wa pembejeo na kuhakikisha kuwa pembejeo zinafika kwa wakati na zinamfikia mkulima katika eneo lake.
4. Wilaya ilipokea pikipiki 10 kutoka kwa makampuni 3 na kuwagawia maafisa ugani ambao hawakuwa na pikipiki kwa ajili ya kusimamia shughuli za pamba.
5. Wilaya ilipata tani 80 za mbegu ya UKM08 ambayo ni mbegu, mpya na bora kwa kuwa inatoa matunda mengi ambayo yanaongeza tija katika uzalishaji na kuhamasisha wakulima.
6. Kupata pembejeo za kilimo kwa muda muafaka kulingana na mahitaji.
7. Kutatua changamoto za kilimo cha pamba kwa haraka kwa kuwa DTF na kampuni huketi kila wiki, kuangalia mapungufu mbalimbali ambayo yanajitokezea na kuyatolea ufumbuzi wa haraka ili kuepuka athari kubwa kwa mkulima.
8. Kurudisha fikra za wakulima katika kilimo cha pamba kwa kuwa pembejeo zimekuwa zinapatikana kwa wakati na kwa urahisi. Takribani 95% ya wakulima waliolima pamba katika msimu huu wamekopa pembejeo.
9. Maafisa ugani wa kata walijengewa uwezo na kampuni ya uzalisha wa mbegu ya Quton

10. Kuanzisha mashamba darasa katika shule za Msingi na Sekondari
11. Tunarajia kuongeza uzalisha kutoka kilo 2,051,122 hadi kufikia kilo 9,610,000

8.0: CHANGAMOTO

1. Upungufu wa mvua kwa mwezi Desemba na Januari ulisababisha wakulima wengi kushindwa kupanda mbegu ya pamba na wengine ambao walikuwa wameshapanda kurudia tena kutokana na mbegu walizopanda mara ya kwanza kutoota kabisa. Baadhi ya wakulima walitelekeza mashamba yao.
2. Zao la pamba kunyauka na kudondosha majani na vitumba ambavyo havijakomaa kutokana na kushambuliwa na wadudu aina ya 'thrips'
3. Upungufu wa maafisa ugani.
4. Kuwa na aina nyingi ya viuadudu katika soko na vingine kutokuwa uwezo wa kuua wadudu kama perfector, Turantura na snowmectic.

9.0: MIKAKATI

1. Kikosi Kazi cha Pamba cha Wilaya kulinda kampuni ambazo zimewekeza kwa kusimamia mikataba ya uwekezaji.
2. Kikosi Kazi cha Pamba cha Wilaya, Makampuni na VTF kudhibiti utoroshwaji na ununuzi pamba holela
3. Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya na Halmashauri kudhibiti utoroshwaji na usafirishaji wa pamba zaidi ya saa 12 jioni.
4. DTF, VTF na Wakulima kusimamia usafi, ubora wa pamba, kudhibiti wizi kupitia mizani, kukusanya takwimu za manunuzi na masafirisho pia kukusanya madeni ya pembejeo zilizokopeshwa vijijini.

10.0: SHUKRANI

Wilaya inatoa shukrani kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwongozo wake thabiti kuhusu kufufua zao la pamba, shukrani kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kutoa maelekezo ya utekelezaji wa agizo hilo, shukrani kwa Bodi ya Pamba Tanzania na TGT kwa ushirikiano wao wa karibu na pia kwa wananchi kwa muamko wao katika kilimo cha pamba. Wilaya inaunga mkono kilimo cha pamba kwa mfumo wa mkataba kwani unamuwezesha mkulima kupata pembejeo kwa wakati halikadhalika uhakika wa soko.

Mhe. Waziri na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, nitumie fursa hii tena kuwakaribisheni tena Wilaya ya Kwimba na pia kuwatakia kila la kheri katika juhudi za kukuza uzalishaji wa zao la pamba.

Eng. Mtemi Msafiri Simeon
Mkuu wa Wilaya
KWIMBA